East African Scholars Journal of Education, Humanities and Literature
*Abbreviated Key Title: East African Scholars J Edu Humanit Lit*
ISSN: 2617-443X (Print) & ISSN: 2617-7250 (Online)
Published By East African Scholars Publisher, Kenya
Volume-8 | Issue-12 | Dec- 2025 | DOI: https://doi.org/10.36349/easjehl.2025.v08i12.001

OPEN ACCESS

**Original Research Article**

# Mbinu Zinazotumika Kuunda Motifu za Safari na Msako Katika Mashairi ya Kimaelezo: Mifano Kutoka Katika Diwani ya *Sauti ya Dhiki* (1973) ya Abdilatif Abdalla

Nkinde Mwangoka[1]*, Prof. Aldin K. Mutembei[2], Elizabeth Godwin Mahenge[3]

[1]Mhadhiri Msaidizi, Chuo Kikuu Kishiriki cha Jordan
[2]Profesa Mshiriki, Idara ya Fasihi, Mawasiliano na Uchapishaji, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
[3]Mhadhiri Mwandamizi, Idara ya Fasihi, Mawasiliano na Uchapishaji, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

**Article History**
**Received:** 16.10.2025
**Accepted:** 08.12.2025
**Published:** 11.12.2025

**Journal homepage:** https://www.easpublisher.com

**Quick Response Code**

**Abstract:** Makala hii inahusu mbinu zilizotumika kuunda motifu za safari na msako katika mashairi ya Kiswahili katika diwani ya *Sauti ya Dhi*ki (1973) ya Abdilatif Abdalla. Makala hii inalenga kuiziba pengo la kiutafiti juu ya mbinu zinazounda motifu, kwani hakuna tafiti zilizofanyika kubainisha mbinu zinazounda motifu za safari na msako katika Ushairi. Katika uga wa fasihi baadhi ya wataalamu wamechambua mbinu mbalimbali za kisanaa zinazounda kazi za fasihi kwa ujumla, na wale walioangalia muundo wa motifu katika kazi za fasihi walibaini hisia ndio kichocheo kikuu kinachosababisha ujirudiajirudiaji wa kimotifu, hivyo basi hisia huunda motifu. Ushairi wa kimaelezo ni miongoni mwa kazi za fasihi zilizo na motifu za safari na msako na zinaundwa kwa miundo bayana. Licha ya tafiti mbalimbali kubaini kwamba motifu hizo zinajitokeza zaidi katika ushairi simulizi na ule wa kidrama. Ombwe la tafiti juu ya mbinu zinazotumika kuunda motifu za safari na msako limekuwa bayana hususani katika mashairi ya kimaelezo. Hali hii ikiachwa bila kuchunguzwa inasababisha kukosekana kwa maarifa kuhusu mbinu zinazotumika kuunda motifu hususani motifu za safari na msako katika mashairi ya kimaelezo. Mashairi ya kimaelezo yaliyorejelewa ni yale yanayopatikana katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* (1973) ya Abdilatif Abdalla. Data za Makala hii zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini wa matini teule wa mashairi ya kimaelezo katika diwani teule. Nadharia za Mwingilianomatini na Ruwaza ya Shujaa ndizo zilizoongoza ukusanyaji na uchambuzi wa data za Makala hii kupitia misingi yake mbalimbali kama itakavyofafanuliwa katika Makala. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa kuna mbinu tano zilizobainika kuunda motifu za safari na msako katika mashairi ya kimaelezo katika diwani teule. Mbinu hizo ni mbinu ya ruwaza, mbinu ya diolojia, mbinu ya shajara, mbinu ya kisitiari na mbinu ya sauti ya usimulizi.

**Keywords:** Motifu, Motifu Ya Safari, Motifu Ya Msako, Mashairi Ya Kimaelezo.

**Copyright © 2025 The Author(s):** This is an open-access article distributed under the terms of the Creative Commons Attribution **4.0 International License (CC BY-NC 4.0)** which permits unrestricted use, distribution, and reproduction in any medium for non-commercial use provided the original author and source are credited.

## 1.0 UTANGULIZI

Dhana ya motifu imefasiliwa na wataalamu mbalimbali kwa namna tofautitofauti. Fasili hizo zinaweza kuwekwa katika makundi matatu. Kundi la kwanza ni lile linalofafanua motifu kwa kujikita katika kigezo cha maudhui, kundi la pili ni lile linaloona motifu ni kama kipengele au dhana ya kifani; kiishara, kimuundo, picha, tendo au sauti. Mbali na makundi hayo mawili, kuna kundi la tatu linaloona motifu kama kipengele cha kifani na kimaudhui Baadhi ya wataalamu katika uga wa fasihi wanafasili motifu kuwa motifu ni kipengele cha kifani au kimaudhui cha kimapokeo ambacho fanani na hata waandishi hukitumia katika kuumba hadithi zao. Aidha, vipengele hivyo huweza kuwa mhusika, ushujaa, tukio, ishara, picha, sauti au tendo linaloonesha ishara maalumu katika hali inayojirudiarudia na kusaidia kukuza na kuendeleza vipengele mbalimbali vya kazi ya fasihi ili kukamilisha maana na kusudi la mwandishi (Freedman, 1971; Mulokozi, 2017; Sosoo, 2018). Kwa hiyo, katika Makala hii dhana ya motifu imetazamwa kama kipengele cha kifani na/au kimaudhui kinachojirudiarudia kwa lengo la kufanikisha dhima fulani.

***Corresponding Author:** Nkinde Mwangoka
Mhadhiri Msaidizi, Chuo Kikuu Kishiriki cha Jordan

Motifu ya safari, wataalamu wengi wanaieleza motifu ya safari kama hali ya kujirudiarudia kwa matumizi ya safari ya kutoka sehemu moja kwenda nyingine, au kukua kiroho, kihisia na kisaikolojia kwa mhusika mkuu akiwa anaendelea mbele kutoka hatua moja ya maisha kwenda nyingine, huku akisaka au akitimiza kitu fulani kitakachomfanya arithike (Nyongesa, 2014; Gichovi, 2016; Mung'aya, 2018). Mathalani, Nyongesa (2014) anadai kuwa motifu ya safari ni matumizi ya safari za mara kwa mara, hususan kwa shujaa, na kile anachokidhihirisha pamoja na njia anayoitumia. Anaendelea kueleza kuwa huo ni mwendo wa kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine. Mwendo huo huunda mandhari, ploti, wahusika na vipengele vingine vya kimasimulizi. Mung'aya, (2018) anaeleza kwamba motifu ya safari ni mwendo wa mhusika au wahusika kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Mwendo huo ni wa kutoka sehemu moja kwenda nyingine ili kukua kiroho, kihisia, kimawazo na kisaikolojia kwa mhusika mkuu au wahusika wengine ndani ya kazi ya fasihi ili kuikomboa jamii. Kutokana na maelezo hayo inabainika kwamba, hali ya uundaji wa vipengele katika hali ya kujirudiarudia unatengeneza kufungamana kwa motifu za safari na msako.

Motifu ya msako, wataalamu wanaifasili kuwa ni ile ambayo shujaa lazima asafiri safari ya hatari kwa ajili ya ukombozi wa watu wake: masimulizi ya safari hiyo yanakuwa ndio ploti ya msingi ya kazi hiyo (Wheeler, 2018; Howard, 2010). Motifu ya msako ni njia ya jaribu ambapo shujaa anasikia mwito na kuondoka nyumbani kwake peke yake au akiambatana na watu wengine kusaka kitu cha thamani. Hii ni ruwaza ya masimulizi ya kawaida katika kazi za fasihi, ambapo shujaa anaanza safari ya kufanikisha lengo fulani au kupata kitu fulani na huku akipambana na majaribu na matatizo njiani (Fiveable, 2024). Akielezea kuhusu dhamira ya safari, Howard (2010) anasema kuwa inaweza kuwa kutafuta maarifa yaliyopotea, kumkomboa rafiki au ndugu aliyetekwa, kutupa mbali kitu kilicholaaniwa au kutafuta kitu cha thamani. Katika safari hiyo, shujaa akiwa njiani anakumbana na matatizo lakini anapata msaada na kupambana na maadui. Shujaa akiwa katika msako huo anaweza kufa, lakini iwapo atafanikiwa kupata kitu cha thamani alichokuwa anakisaka; anabadilika, hatakuwa sawa na alivyokuwa kabla ya kuanza safari. Hivyo basi, Makala imebaini kwamba motifu ya msako ni ile ambayo uwepo wake unategemea uwepo wa safari yenye lengo maalumu la shujaa na au mhusika yeyote ndani ya kazi ya fasihi. Aidha, imeonekana pia kuwa kuna uwezekano wa karibu wa motifu hizo kutegemeana au kuhusiana. Hali hiyo inazua kuwapo kwa mitazamo tofautitofauti kuwa motifu hizo zinapaswa kutazamwa kama kitu kimoja au vitu viwili tofauti.

Mashairi ya kimaelezo, ni aina ya mashairi ambayo kiasili tangu Aristotle alipoandika kitabu chake cha Poetics yaliainishwa pamoja na mashairi ya kimasimulizi na mashairi ya kidrama kama aina au tanzu muhimu za mashairi (Hurley, O'Neill, 2012). Mashairi ya kimaelezo yanatokana na neno lyric la Kiingereza ambalo lina asili ya neno la Kigiriki Lurikos/lyre likihusianishwa na muziki na udhihirishaji wa hisia kali (Brewster, 2009). Mashairi ya kimaelezo ni utanzu unaohusu maisha binafsi: ni yale tunayoyaongea peke yetu tukiwa wenyewe. Mashairi haya yanaongelewa na muongeaji akiwa peke yake, na yule anayeongeleshwa mara nyingi ni Mungu au mtu wa karibu na muongeaji ambaye hayupo karibu (Vendler, 2002). Aina hii ya ushairi inamuumba mtunzi zaidi ya mtunzi kuumba ushairi, sababu inazungumza juu ya hisia za ndani za mtunzi, hivyo mtunzi kupata nafasi ya kubadilika (Hurley, O'Neill, 2012). Katika Makala hii, mashairi ya kimaelezo yamefasiliwa kama mashairi yanayotoa maelezo kuhusu kitu, jambo au hisia zake za ndani. Mashairi haya yanadhihirisha sifa za kimuziki, lakini yanaandikwa kwa lengo la kusomwa au kughanwa sio kuimbwa

## 2.0 METHODOLOJIA YA UTAFITI

Data za Makala hii zilikusanywa kwa njia ya usomaji. Hivyo basi, mbinu ya usomaji matini na uchambuzi matini zilitumika ili kutimiza lengo la makala hii. Data za utafiti huu zilikusanywa kutoka katika mashairi ya kimaelezo katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* (1973) ya Abdalatif Abdalla kwa kutumia mbinu ya usomaji matini. Diwani hiyo ilipatikana kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa. Aidha, diwani hii iliteuliwa kutokana na ni kuona mashairi yenye mguso wa hisia zenye mfungamano na safari au msako fulani. Upatikanaji wa data hizo ulifanyika maktabani kwa kutumia njia ya usomaji matini na uchambuzi matini. Data zilizokusanywa kutoka katika diwani teule ziliwasilishwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli.

## 3.0 KIUNZI CHA NADHARIA

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Ruwaza ya Shujaa kwa kufuata ruwaza mahususi pamoja na Nadharia ya Mwingilianomatini. Nadharia ya Ruwaza ya Shujaa ni Nadharia ya Umuundo ambayo inaibua masuala ya kimuktadha na kihistoria. Nadharia hii iliasisiwa na Von Hahn (1876) ambaye alitoa ruwaza ya kwanza ya shujaa. Msingi wa nadharia hii ni hatua mbalimbali za ukuaji wa shujaa tangu kuzaliwa kwake, kusafiri nchi za mbali, kufundwa, kukomaa, kurejea na kupata ushindi. Maelezo haya yaliendelezwa na wanazuoni mbalimbali, wakiwemo Raglan (1956), Rank (1959), De Vries (1963), Propp (1968) na Campbell (1973). Wanazuoni hawa waliandaa orodha za ruwaza za mashujaa kutoka katika jamii za Ulaya na Asia. Kundi lingine la wanazuoni walioandika kuhusu nadharia hii ni Biebuyck (1969, 1978), Bird (1978, 1977), Okpewho (1979), Kunene (1980), Mbele (1986), na Johnson (1978, 1986). Kundi hili liliona kuwa ruwaza za mwanzo hazijitoshelezi katika uainishaji wa ruwaza ya shujaa wa utendi wa Kiafrika.

Kwa upande wa Nadharia ya Mwingilianomatini ni Nadharia inayotumika

kumaanisha uhusiano na mgongano kati au ndani ya matini moja au zaidi. Matini inaweza kuwa ya maandishi au masimulizi ya mdomo. Uhusiano huo huanzia katika nukuu, uelezwaji wa jambo moja na jingine na hata kuwa na lugha zinazofanana au kuhusiana. Nadharia ya Mwingilianomatini iliasisiwa na Julia Kristeva miaka ya 1960; na ni matokeo ya Nadharia ya Ferdinand de Saussure (1857) ya Umuundo na Nadharia ya Mikhail Bakhtin (1895) ya Usemezano.

## 4.0 UCHAMBUZI NA UWASILISHAJI WA DATA

Sehemu hii inahusu uchambuzi na uwasilishaji wa data zilizopatikana katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* (1973). Uwasilishaji na uchambuzi wa data uliongozwa na mihimili ya nadharia za Ruwaza ya Shujaa na Nadharia ya Mwingilianomatini kama ilivyodokezwa hapo awali. Utafiti uliozaa makala hii, umebainika kwamba mwandishi ametumia mbinu mbalimbali kuunda motifu za safari na msako katika diwani hii ya *Sauti ya Dhiki* (1973). Mbinu hizo zinajadiliwa zikiongozwa na Nadharia ya Ruwaza ya Shujaa kwa kuandika mashairi kwa kufuata ruwaza mahususi pamoja na Nadharia ya Mwingilianomatini ambapo kuna mwingiliano wa tanzu zingine za fasihi na sifa zinazounda tanzu zingine za fasihi tofauti na mashairi. Mbinu hizi zinabainishwa mojamoja na kufafanuliwa zikirejelea mashairi ya kimaelezo yaliyobeba motifu husika katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* (1973) Abdilatif Abdalla. Katika utafiti huu haijabainika tafiti zilizochambua mbinu za uundaji wa motifu za safari na msako. Mbinu hizi zimejadiliwa zikiongozwa na misingi ya hatua anazozipitia shujaa katika safari yake kama alivyozibainisha Campbell, (1973) pamoja na Mulokozi (2017) katika Nadharia ya Ruwaza ya Shujaa. Pia imetumika misingi ya Nadharia ya Mwingilianomatini kama udialojia pamoja na Ukanivali ambao ni usawiri wa kifasihi unaotumia dhihaka na kejeli kusawiri maovu yaliyomo katika jamii. Mbinu hizo zimefafanuliwa kama zifuatazo:

### 4.1 Mbinu ya Ruwaza

Mbinu ya ruwaza ni mbinu ambayo inategemea matumizi ya namna jambo fulani, umbo, mistari au rangi inavyojitokeza au kufanyika kwa kujirudiarudia (BBC, 2025). Katika diwani hii ya *Sauti ya Dhiki* (1973), mwandishi ametumia ruwaza kama mbinu mojawapo ya kuunda motifu. Mfuatano wa visa vilivyojenga motifu ya safari ya mwandishi katika viwango mbalimbali vinaweza kubashiliwa kwa kufuata kanuni ya ruwaza ya shujaa ingawa imejitokeza katika mashairi ya kimaelezo na si masimulizi kama ilivyozoeleka.

Mashairi yamepangiliwa kwa kiasi kikubwa kisafari ya ndani huku yakionesha mabadiliko ya mwandishi kisaikolojia. Mwandishi anapitia hatua mbalimbali za mabadiliko ambayo yako kiruwaza. Kama ambavyo Campbell (1973) anafafanua katika Nadharia ya Ruwaza ya Shujaa, anaeleza hatua tatu za ruwaza ambazo humtokea shujaa wa tamaduni zote ulimwengu. Mwandishi katika diwani hii amepitia hatua hizo katika mashairi ya kimaelezo. Maisha ya mwandishi kabla ya kifungo yamekuwa na athari kubwa katika maisha ya kifungo. Lakini pia, matamanio ya mwandishi kabla ya kifungo yamekuwa na athari katika maisha ya baada ya kifungo akiwa huru.

Campbell anazigawa hatua za ukuaji wa shujaa katika madaraja matatu: kujitenga (separation) kufundwa (initiation) na kurejea (return). Mwandishi Abdilatif Abdalla katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* (1973) ameonesha safari aliyoipitia kifungoni huku akipitia hatua hizi tatu. Katika safari hii ya mwandishi, motifu za safari na msako zimeundwa kwa namna mbalimbali.

Mbinu hii ya uandishi wa mashairi kwa kutumia ruwaza ya shujaa imejidhihirisha kwa mpangilio wa mashairi yanayoendana na nyakati na matukio aliyopambana nayo siku baada ya siku au siku kadhaa ndani ya mwezi katika kipindi chote akiwa kifungoni. Mwandishi aliandika mashairi kwa kutumia mbinu ya shajara, ambapo aliandika tarehe ya kila shairi alipoliandika. Hivyo, ni rahisi kufuatilia safari yake na mabadiliko ya mtazamo wake juu ya lengo kuu la safari. Katika mabadiliko hayo ya mtazamo wa mwandishi, ndipo inaonekana jinsi motifu zilivyoundwa. Katika mbinu hii, motifu iliyotawala ni motifu ya safari ambayo ina msako ndani yake, pia kuna safari isiyo na msako kwa kiasi kidogo.

Safari iliyo na msako imeundwa kwa kufuata safari kuu ya mwandishi kuipambania kweli pamoja na safari ya serikali kumfunga mwandishi kwa lengo la kumbadilisha mawazo yake. Safari hizi zinajionesha bayana katika mashairi yafuatayo: 'N'shishiyelo ni Lilo', 'Siwati', 'Kamliwaze', 'Jipu', 'Telezi', 'Ah! Mwenzangu', 'Kokoiko', 'Wasafiri Tuamkeni', 'Zindukani' na 'Mamaetu Afrika'. Pia, kuna safari zenye misako mingine midogomidogo ambazo zimejitokeza ndani ya safari hizi kuu mbili. Safari hizo ni kama: kwanza, ni safari ya wapigania kweli wa zamani waliopitia shida na misukosuko kama ilivyo kwa mwandishi wa diwani hii. Safari hii inapatikana katika shairi la 'Kamliwaze' na 'Siwati'. Pili, kuna safari ya mapenzi ya mwandishi na mpenzi wake, ndugu zake pamoja na rafiki zake. Hii inapatikana katika mashairi ya 'Nakukumbuka', 'Linalokuudhi ni Lipi' na 'Watiliye Pamba'.

Safari isiyo na msako ambayo pia ni safari ndogo iliyojitokeza ndani ya safari kubwa ya mwandishi ni safari ya mtumishi katika shairi la 'Kamliwaze'. Katika safari hii, mtumishi anatimiza lengo la bwana wake na hana hiari. Anasafiri kwa lazima. Hii ni aina ya safari ambayo inatimiza msako wa mtu tofauti na asafiriye. Ni safari ya kitumwa. Pia, kuna safari ya kifungo ya mwandishi wa diwani hii ya *Sauti ya Dhiki* (1973) kwa kiasi fulani, nayo ni safari isiyo na msako kwa mwandishi. Hii ni safari iliyoanzishwa na serikali ya Kenya ilipomtia hatiani mwandishi na kumpa hukumu ya

kifungo cha miaka mitatu jela. Hukumu hii aliyopewa mwandishi katika siku za mwanzo za kifungo chake aliwekwa katika chumba cha peke yake, bila kalamu wala kitabu. Mwandishi anasema lengo lao lilikuwa kumuumiza ili abadilike pindi arudipo uraiani. Huu ulikuwa msako mkuu wa serikali. Mwandishi kwa upande wake hakuwa na uchaguzi, alipaswa kufuata maelekezo ya waliomfunga. Katika shairi la 'Telezi' mwandishi anaonekana akijuta kutumia njia aliyoitumia kwani ilimuumiza zaidi kuliko kumsaidia. Hii inamaanisha kwamba kwa kiasi fulani msako wa serikali ulifanikiwa. Ingawa katika mashairi mengine alionesha kutokata tamaa na kutobadili msimamo wake. Kwa mfano, alidhihirisha hilo katika shairi la 'Siwati'.

Kwa kutumia mbinu hii ya uandishi, utafiti huu umeweza kufuatilia motifu ya safari ya mwandishi akiwa kifungoni katika hali tofauti tofauti pamoja na safari nyingine zilizojitokeza katika mashairi ambazo pia zilikuwa zinashadadia safari ya mwandishi.

Katika maelezo ya mwandishi, inafahamika kwamba kabla ya kupewa kalamu ya kuandikia, mwandishi alipitia mateso mengi kwa ajili ya kumbadilisha msimamo wake dhidi ya serikali. Mwandishi alifungiwa chumba cha peke yake akiwa na ulinzi muda wote, hakuruhusiwa kuchangamana na wafungwa wenzake wala kusoma na kuandika. Mwandishi alichoka sana na kuumia kisaikolojia, lakini hali hii ya kuchoka na kuumia haionekani kama ilimsaidia mwandishi kukata tamaa na kubadili mawazo juu ya msimamo wake katika kusema kweli. Imani na mtazamo wa mwandishi juu ya kusema kweli kama ilivyokuwa kabla ya kuingia kifungoni unajidhihirisha vilevile katika mashairi yake ya mwanzo tofauti na ilivyotarajiwa na waliomweka kifungoni, na kumpitisha kwenye mateso makali. Katika shairi lake la kwanza la 'N'shishiyelo ni Lilo', mwandishi ameanza kwa kueleza sababu ya kufungwa kwake na hali ya mateso aliyopitia ya kifungo kikali. Mwandishi anaeleza kwamba kusema kwake kweli kumemfanya apitie maumivu mengi ya moyoni na mwilini. Mwandishi anasema:

Kweli yanipasha tabu, ndugu yangu niamini
Na nyingi mno adhabu, za moyoni na mwilini
Yote hayo ni sababu, ya kunena kweli hini
Ndipo sasa huamini, kweli i utungu kweli. (ub. 7)

Mwandishi anaeleza matatizo mengine mengi aliyoyapata akiwa kifungoni ikiwa ni pamoja na kutengwa na ndugu zake, kwa kufungiwa chumba cha peke yake akiwa na ulinzi mkali. Pia, mambo mengine aliyoyalalamikia mwandishi ni kulala chini kwenye sakafu yenye baridi kali, kutochangamana na wafungwa wenzake, kunyimwa haki ya kusalimiwa na ndugu zake wala kuandika na kuletewa barua. Ingawa mwandishi alipitia mateso yote haya lakini anaeleza kuanzia ubeti wa kumi na tatu mpaka ubeti wa mwisho (ishilini na moja) kwamba ingawa alitendewa yote hayo kwa lengo la kumbadili nia lakini hatakuja kuacha kusema kweli. Kwa mfano, katika ubeti wa kumi na tano na kumi na tisa mwandishi anasema:

Mno wangeniadhibu, adhabu kila namna
Na mangi yanganiswibu, ya usiku na mtana
Hayakuwa sababu, ya kuniasa kunena
Kweli nitapoiyona, tanena siinyamai (ub 15)

Wangi washasumbuliwa, waneni wa kweli hiyo
Na wangi washauliwa, kwa kutobadili nyoyo
Na mimi nimeradhiwa, kuyandama sera hiyo
'Tafuwata zao nyayo, n'shishiyelo ni lilo. (ub. 16)

Kwa kutumia mbinu hii ya shajara, imebainika hali ya mwandishi kuanzia shairi la kwanza mpaka shairi la mwisho la kimaelezo aliyoyaandika akiwa kifungoni. Utafiti huu umeweza kufuatilia safari ya nje, ya ndani (kisaikolojia) na safari ya kisitiari ya mwandishi katika kupigania kweli. Pia, umefuatilia safari ya mapenzi kwa ndugu, marafiki, jamii na mpenzi wake kama ilivyoelezwa katika sura ya tano. Safari hizi za mwandishi zinatoa picha halisi ya hatua tatu za safari ya shujaa alizozieleza Campbell (1973). Mfuatano wa visa vilivyojenga motifu ya safari ya mwandishi katika viwango mbalimbali vinaweza kubashiliwa kwa kufuata kanuni ya ruwaza ya shujaa ingawa imejitokeza katika mashairi ya kimaelezo na si masimulizi au kama ilivyozoeleka.

Katika hatua hizi, utafiti huu unamuona mwandishi katika hatua ya kwanza akijitenga au kutengwa kwa kupelekwa kifungoni. Katika hatua hii, mwandishi hakuwa na hiari. Alianza safari kwa kulazimishwa. Ingawa mwandishi alijua kuwa kuandika kwake kweli kungeweza kumsababishia matatizo alikuwa tayari kukabiliana nayo pale yatakapompata. Lakini inaonekana baada ya kupata mashtaka, mwandishi alipambana kujinasua peke yake.

Hatua nyingine aliyoieleza Campbell ni hatua ya kufundwa. Katika hatua hii, mwandishi anaonekana akipitia maumivu na kukatishwa tamaa akiwa kifungoni, ikiwa ni pamoja na kupoteza ndugu na rafiki zake kwa sababu ya kifo, kusalitiwa, kuhamishwa gereza na kusahauliwa. Mwandishi alipitia maumivu mengine mengi ambayo wakati mwingine yalimkatisha tamaa lakini baadaye aliinuka na kujipa moyo huku akikumbuka lengo la safari yake na msimamo wake.

Mwisho, mwandishi anapitia katika hatua ya tatu ya kurejea. Mwandishi anaeleza jinsi alivyokomaa kuliko ilivyokuwa mwanzo. Mwandishi anaonesha hatua ya pili ya kufundwa ilivyomkomaza, hivyo anarejea akiwa na nguvu zaidi kuliko awali. Amethibitisha hali hiyo katika shairi la 'Naja'. Mwandishi anasema:

Naja hiwa 'mekomaa, kuzidi nilivyo mwando
Tena nnajiandaa, kwa fikra na vitendo
Kwetu nije kuifaa, na kuitiliya pondo
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini (ub. 6).

Katika dondoo hilo, mwandishi anajiamini, hana hofu tena. Hatua ya kufundwa aliyoipitia inaonesha imefanikiwa. Hata akianza safari ya kurudi, uhakika wa shujaa kuweza kutawala akifika nyumbani, ni mkubwa. Hivyo basi hatua tatu za ruwaza ya shujaa alizozieleza Campbell zimejitokeza dhahiri shahiri katika diwani hii. Mbinu hii ambayo imeelezwa kuwa inapatikana katika kazi za fasihi za kimasimulizi (Mulokozi, 2017; Kunene, 1985), lakini imeonekana imeweza pia kutokea katika mashairi ya kimaelezo. Pia, mbinu hii imejidhihirisha katika safari ya ndani ya mwandishi tofauti na ilivyozoeleka kujitokeza katika safari ya nje katika kazi za fasihi za kimasimulizi.

**4.2 Mbinu ya Diolojia**

Diolojia ni dhana iliyoanza kutumiwa na Plato akifafanua kuwa ni kazi za kilahaja za Socrates zinazodhamiria kuwasilisha mawazo ya kifalsafa kwa kujibizana (Pfister, 1998). Anaendelea kueleza kwamba kwa mujibu wa Aristotle dhana hii ni moja ya vipengele vinavyoikamilisha kazi ya fasihi, ikiwa ni majibizano ya wahusika ambayo yamebeba; muktadha, sauti, toni, mandhari pamoja na migogoro ya wahusika. Pia, haya ni mawasiliano kati ya wahusika pamoja na mjadala wa nafsi anaoweza kuwa nao mhusika mmoja. Dhana hii imeendelezwa na wataalamu wengi wakiwemo; Shakespeare, Bakhtin na kadhalika. Tofauti na mawazo ya wataalamu hawa, katika utafiti huu tumebaini kwamba, diolojia sio lazima yawe majibizano ya wahusika tu, bali pia inaweza kuwa majibizano ya waandishi, wawasilishaji au kazi za fasihi juu ya dhana au dhamira moja. Matokeo ya utafiti huu yamebaini kwamba, mbinu ya diolojia imetumika kuunda motifu za safari na msako katika mashairi ya kimaelezo katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* (1973) Abdilatif Abdalla. Mbinu ya diolojia iliyotumiwa na mwandishi ni kama anavyoeleza Kristeva (1980) kwamba neno hupata uhai kwa sababu lina uhusiano na neno lingine na muktadha fulani. Uhai huu hupatikana kati ya mpaka wa neno moja na lingine. Hivyo, maana haipatikani katika neno au matini moja tu bali katika mkutano wa usemezano na mwingiliano wa sauti mbalimbali. Katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* (1973), diolojia ya matini imejitokeza kwa namna mbalimbali, na diolojia hii imeunda motifu za safari na msako.

Utafiti umebaini kwamba kuna mashairi ambayo yamekuwa yakiitikiana katika dhamira mbalimbali. Hii ni diolojia tofauti na ile iliyofafanuliwa na Pfister, (1998) kwani, mwandishi ametunga mashairi ambayo ni majibu ya mashairi au barua alizotumiwa na ndugu zake. Mashairi haya yapo ambayo yameelezwa bayana na mwandishi mwanzoni mwa kitabu katika dibaji, pia yapo ambayo hayajaelezewa na mwandishi lakini dhamira zake zinazomtaka msomaji au mlengwa atoe majibu. Baadhi ya mashairi ambayo yalitungwa kwa kutumia mbinu ya diolojia ni shairi la ‘Tuza Moyo’. Mwandishi anasema alitunga shairi la ‘Tuza Moyo’ kujibu shairi aliloletewa na mmoja kati ya waliomuonea huruma. Shairi hili linapatikana katika dibaji ya diwani ya *Sauti ya Dhiki* (1973) (xiii) shairi linasema:

Subira huvuta kheri, ukisubiri ni mno
Nawe zidi kusubiri, wekeze mbingu mikono
Uombe alo Qahari, inshallah hukosi neno
Ushike wosia huno.

Baada ya mwandishi kupata shairi hili lenye ubeti mmoja tu wenye mishororo minne, alijibu kwa kutunga shairi la ‘Tuza Moyo’ ambalo nalo lina ubeti mmoja wenye mishororo minne tu. Katika shairi hili mwandishi anasema:

Akhi tuliza mtima, uwate kusononeka
Hakuna lisilokoma, siku ‘kifika’ tatoka
Kusubiri ni lazima, na kumuomba Rabbuka
Wasiya wako’ meshika

Katika beti hizi mbili mbinu ya udiolojia imejibainisha kwa waandishi wawili kujibizana kwa kupitia mashairi yao. Udiolojia huu unashadadia uundaji wa motifu za safari na msako wa maisha ya mwandishi kifungoni na motifu ya safari na msako wa kusaka kweli. Katika shairi la kwanza mwandishi alipewa wosia, huku akisisitizwa awe na subira na akimtegemea Mungu; kisha, naye alijibu kuwa wosia ameushika, lakini pia anamsihi atulize moyo kwamba ipo siku atatoka lakini lazima wawe na subira. Katika shairi hili, mwandishi anaonesha muundo wa motifu ya safari ya mwandishi yenye lengo na matumaini. Mwandishi anaamini kuwa kila lililo na mwanzo halikosi mwisho. Jambo la msingi ni subira na kumuomba Mungu.

Mwandishi anaendelea kutumia mbinu ya diolojia kuunda motifu za safari na msako katika mashairi yake, anaeleza kwamba shairi la ‘Sikakawane na Kimya’ alimtungia kaka yake Ahmadi wa Nasiri (Ustadhi Bhalo) kutaka kujua kwa nini hamtumii barua. Aina hii ya udiolojia unaendana kidogo na ule anaoulezea Mulokozi (2017) katika aina za ushairi, hususani ushairi wa maigizo ya kingonjera. Ingawa katika ngonjera majibizano huwa kuna pande mbili zinazojibizana kuhusu jambo fulani ndani ya shairi moja. Matokeo ya utafiti huu yamebaini majibizano sio lazima yajitokeze ndani ya kazi moja ya fasihi bali yanaweza kujitokeza kati ya watunzi wawili au zaidi. Katika shairi hili linaloonesha mbinu ya diolojia aliyoitumia mwandishi katika kuunda motifu. Shairi hili linatoa picha ya diolojia iliyokuwepo kati ya mwandishi na ndugu yake kabla ya utunzi wa shairi hili pia jinsi diolojia hiyo ilivyo katishwa na upande mmoja kutotoa majibu. Katika shairi hilo mwandishi anasema:

Ndugu yangu Ahmadi, kwani kunitenda haya?
Kimya chako kimezidi, hata kimeshapindukiya
Leo hawa sina budi, ila kukiuliziya
Kimya kingi ni kibaya, usikakawane nacho (ub. 1)

Nyaraka nikweteyazo, ambazo hukufikiya
Na salamu niwapazo, watu ili kukweteya
Hujishughulishi nazo, japokuwa mara moja
Kimya kingi ni kibaya, usikakawane nacho. (ub. 2)

Katika dondoo hili linaonesha uwepo wa diolojia iliyokatishwa ambayo inashadadia ujenzi wa motifu ya safari na msako wa maisha ya mwandishi akiwa kifungoni pamoja na motifu za safari na msako wa kweli. Ambapo safari yamaisha ya mwandishi kifungoni inaleta kiu na msako wa faraja na kujenga mahusiano na ndugu zake. Mwandishi hataki kifungo kisababishe kuvunjika kwa ukaribu alionao na ndugu yake. Mwandishi anamuuliza ndugu yake kama kuna tatizo lolote linalosababisha ukimya huo. Katika ubeti wa 5 na 6, mwandishi anamsihi amwandikie na yeye kwa kusema:

Nakusisitiza tena, kabla sijatuliya
Kimya hakina maana, kwani wakishikiliya?
Safari hii kazana, upate niandikiya
Kimya kingi ni kibaya, usikakawane nacho. (ub. 5)

Salamu kwako nyumbani, kwa mama na fursiya
Na watu wote uwani, wajuze yangu afiya
Na jamaa mitaani, wa Kuze na Dundee piya
Waambiye nawaambiya, ‘takuwa nao wakani. (ub. 6)

Dondoo hapo juu zinaonesha mahusiano yaliyopo baina ya watu walio katika diolojia hii. Mwandishi katika ubeti wa sita anaendelea kumsihi ndugu yake apeleke salamu kwa ndugu zake nyumbani. Hapa, mwandishi anatuma ujumbe kwa kaka yake Ahmadi lakini wakati huohuo anataka ndugu yake apeleke ujumbe kwa ndugu zake wengine. Majibizano ya kidiolojia hayategemewi kuishia kati ya watu wawili tu katika shairi hili, bali kwa watu wengi zaidi. Shairi hili ni kama barua aliyoiandika mwandishi kwa kaka yake, yenye salamu kwa ndugu wengine. Mwandishi anasema:

Mwandishi katika mshororo wa mwisho wa beti ya sita anasema, ‘Waambiye nawaambiya’ hii inadhihirisha diolojia iliyokuwepo kati ya mwandishi na ndugu yake Ahmadi lakini pia katuma taarifa kwa watu wengine wengi zaidi kupitia kwa ndugu yake. Mwandishi ana matumaini na anatoa taarifa juu ya safari yake ya kifungo kuwa inakaribia kuisha huku akisaka amani na uhusiano mzuri na ndugu zake.

Matokeo ya utafiti huu yamebaini aina muundo mwingine wa diolojia uliojitokeza katika diwani hii. Hii ni diolojia iliyo na muundo wa hotuba usio rasmi. Mulokozi (2017) yeye anaeleza kwamba, hotuba ni mazungumzo rasmi ambayo huwasilishwa kwenye vikao rasmi vya kimila, kisiasa, kidini n.k. Katika diwani hii, mwandishi alitumia mbinu ya diolojia katika kuunda motifu za safari na msako katika shairi la ‘Zindukani’. Katika shairi hili, mwandishi anaongea na watu wa Pwani kwa namna ya kuwahutubia. Lengo la mwandishi ni kuwaonya watu hao; ambao ni wavivu, wanategemea mali za urithi na wenye kupenda usultani, lakini wanafanyakazi ya kuwasema walio navyo ambao wamevipata kwa jasho na kujinyima. Mwandishi hatumii nafasi aliyonayo kuandika juu ya maisha yake tu bali kwa kutumia mishingi ya nadharia ya Mwingilinomatini tunaona mashairi yake yamekuwa mwitiko wa mambo ya kiutamaduni yanayoendelea katika jamii yake (Kristeva, 1980). Katika shairi hilo, matumizi ya nafsi ya kwanza umoja, nafsi ya kwanza uwingi na nafsi ya pili uwingi na tatu uwingi katika beti ya kwanza na beti zingine, yanadhihirisha uwepo wa diolojia. Inaonekana kuwa mwandishi anazungumza na kundi la watu ingawa hauonekani mwitiko wa upande wa pili, lakini inaaminika kwamba, ujumbe uliotolewa na mwandishi umempata yeyote yule aliyesoma shairi husika na mwitiko wake unatokana na maana msomaji aliyolipa shairi husika, ikiwa ni kwa kubadilika, kufurahia, kubeza na kadhalika. Mwandishi anasema:

Sikuja weka baraza, au hadithi kutowa
Sikuja kuzungumza, maneno yasiyokuwa
Nnakuja kuw’eleza, ambayo yatusumbuwa
Tuyatafutiye dawa, twongokewe maishani (ub. 1)

Katika dondoo hili tunaona mwandishi akianzisha diolojia ambayo imeunda motifu za safari na msako wa wasafiri kama ilivyofafanuliwa katika sura ya nne. Katika diolojia hii mwandishi anabainisha hali wanayokabiliana nayo na namna ya kujikomboa. Mwandishi anaeleza jinsi watu wa Pwani akiwemo yeye mwenyewe wanavyoweza kupiga hatua na kuachana na umaskini. Katika ubeti wa mwisho mwandishi anasema:

Hii ni kweli ambayo, hata’mi imeniumiza
Kwamba mbwa sehemu hiyo, kweli hii yaniliza
Yauliza wangu moyo, wala hautanyamaza
Hakuna cha kuupoza, mpaka twondoke tini. (ub. 24)

Katika dondoo hili mwandishi anaonesha imani aliyonayo katika mabadiliko ndani ya jamii yake ipo katika nyanja mbalimbali. Kwanza kabisa katika safari kuu ya mwandishi ndani ya diwani hii, mwandishi ana safari na msako wa kupambana na kusimamia kweli na kuiimarisha katika jamii yake. Lakini katika shairi hili mwandishi anaongeza jambo lingine la muhimu la kimabadiliko katika jamii yake ambalo ni ndani ya safari ya mwanadamukama ilivyofafanuliwa katika sura ya nne anaibua safari ya mabadiliko ya kifikra hususan kwa watu wa Pwani, ili kuachana na umaskini.

Mwandishi ametumia mbinu ya diolojia kuunda motifu za safari na msako katika kutunga shairi la ‘Kwa Heri’. Mwandishi anasema, alitunga shairi hilo kwa ajili ya kumuaga mfungwa mwenzake aliyeitwa Israel Otieno waliyepatana sana wakiwa gerezani. Alitunga kumuaga alipohamishwa kutoka Gereza Kuu la Kamiti kupelekwa Gereza la Shimo la Tewa. Diolojia iliyojitokeza katika shairi hili ni maongezi ya upande mmoja. Kama ilivyo katika shairi la ‘Zindukani’, diolojia hii ipo katika muundo wa hotuba aliyoieleza Mulokozi (2017) ingawa si rasmi. Katika shairi hili matumizi ya nafsi ya kwanza umoja, nafsi ya kwanza uwingi na nafsi ya pili umoja ni moja ya vithibitisho vya matumizi ya diolojia katika shairi hili. Kwa mfano katika ubeti wa kwanza mwandishi anasema:

Nakuaga ndugu yangu, kwa heri ya kuonana
Naondoka nenda zangu, hiwa na simanzi sana

Simanzi moyoni mwangu, kwa tulivyozoweyana
La kutenda ndilo sina, ela kwenenda nendako (ub. 1)

Katika dondoo hili tunamwona mwandishi akiongea na rafiki yake akionesha simanzi aliyonayo kuachana naye. Matumizi ya diolojia katika shairi hili yameonesha kuwepo kwa motifu ya safari ya nje ya mwandishi, ambapo mwandishi alihama kutoka gereza moja kwenda lingine. Ingawa mwandishi hataji moja kwa moja kuwa anaondoka gereza hili kwenda lingine, lakini anaaga kwamba anaondoka. Kuwepo kwa safari hii kunatokana na kuwepo kwa safari kuu ya kusaka na kuisimamia kweli kwa mwandishi, ambayo ndiyo sababu kuu ya kuingia kifungoni. Diolojia hii inasaidia kuunda motifu za safari na msako wa mwandishi kutoka gereza moja kwenda gereza lingine pamoja na motifu ya safari na msako wa mapenzi. Diolojia hii inaonesha safari hizi zinavyoibuliwa kwa sehemu au kwa ukamilifu. Kwani motifu ya safari na msako wa mwandishi wa kweli, maisha ya kifungoni na safari na msako wa mapenzi ni motifu ambazo zimekamilishwa kwa upana kwa kutumia mashairi mbalimbali kama ilivyoelezwa katika sura ya nne. Lakini diolojia inayounda safari na msako wa mwandishi kutoka gereza moja kwenda lingine inakamilika katika matumizi ya shairi hili moja.

Shairi lingine alilolitunga mwandishi kwa kutumia mbinu ya diolojia iliyoumba motifu za safari na msako ni shairi la 'Naja'. Katika shairi hili mwandishi alilitunga kwa nia ya ujumbe uwafikie watu fulani mahususi, huku likitengeneza mbinu ya diolojia. Mbinu ya utunzi wa shairi hili ni kama aliyoitumia wakati alipoongea na watu wa Pwani kupitia shairi la 'Zindukani'. Mwandishi anatoa hotuba isiyo rasmi akizungumza na makundi mawili tofauti. Shairi hili, mwandishi anasema kuwa alilitunga miezi mitatu kabla ya kuachiwa huru. Katika shairi hili, mwandishi anazungumza na wale waliokuwa wakimtakia kheri na wale waliokuwa wakimwombea mabaya. Katika ubeti wa saba na nane, mwandishi anasema:

Naja munaoningoja, kwa vigele na misondo
Ningojeyani 'takuja, nyuso z'ondoweni kundo
Tuje pigana pambaja, wangu wenza wazalendo
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini (ub. 7)

Naja na ambao kwamba, mwaningoja kwa vihendo
Wazidi kukaza Kamba, wasizibadili nyendo
Wangajiita ni simba, sitazicha zao kondo
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini (ub. 8)

Katika dondoo hili, yanaonekana matumizi ya nafsi ya kwanza umoja, nafsi ya kwanza wingi, nafsi ya pili wingi na nafsi ya tatu wingi. Mwandishi anazungumza na makundi mawili tofauti, wale walio na mtazamo kama wake na wale walio dhidi yake. Diolojia hii inadhihirisha uundaji wa motifu za safari na msako. Mwandishi anaonesha safari na msako wa nje wa maisha ya mwandishi kifungoni, akiwa katika hatua ya kurudi nyumbani kama Campbell (1973) anavyoeleza. Pia, anaonesha safari na msako wa ndani wa mwandishi wa kusaka kweli; mwandishi anaonesha jinsi alivyokua na kuboresha msimamo wake alioingia nao kifungoni huku akiwa na moyo safi wa msamaha kwa waliomtenda uovu. Katika ubeti wa kumi mwandishi anasema:

Naja na ingawa naja, siwaekei mifundo
Moyo wangu ushatuja, mawi nalotendwa mwando
Ela wataoningoja, na vyao viwi vitendo
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini (ub. 10)

Katika dondoo hili utafiti unamwona mwandishi akitangaza msamaha kwa wale waliomkosea na kusababisha kifungo chake. Lakini katika mishororo miwili ya mwisho bado anaendeleza diolojia kwa kutoa tahadhari kwa wale ambao bado wana nia ovu juu yake.

Shairi lingine lililotumia mbinu ya diolojia kuunda motifu za safari na msako ni shairi la 'Ah! Mwenzangu'. Katika shairi hili, mwandishi anazungumza na rafiki yake wa karibu sana, ambaye anamuona ni kama ndugu yake waliotoka tumbo moja. Mwandishi anajaribu kumuonya juu ya vitendo vyake kwani vinamvunjia heshima na mwisho wake ni mbaya. Katika shairi hili mwandishi anaonesha mbinu za kuunda motifu za safari na msako wa kusaka kweli. Katika ubeti wa kwanza na wa pili, mwandishi anasema:

Pulika wangu rafiki, rafiki nipulikiza
Kukunasihi sichoki, ingawa wanipuuza
Ijapokuwa hutaki, nasaha kuisikiliza
Ufanyayo ni ya pweza, kujipalia makaa (ub.1)

Maadamu u mwenzangu, nilokuswafiya niya
Wewe kama ndugu yangu, tulotoka tumbo moya
Huwa wanipa matungu, utendapo jambo baya
Sina budi kukwambiya, wajipalia makaa. (ub. 2)

Katika dondoo hili mwandishi anazungumza na rafiki yake wa karibu sana, huku akimpa ushauri juu ya mwenendo wake. Katika wosia huu, mwandishi haelezi bayana rafiki huyo ni nani na amefanya kitu gani. Pia, haielezwi huyo rafiki ameupokeaje ujumbe wa mwandishi. Diolojia hii ni kama iliyojitokeza katika shairi la 'Zindukani' na shairi la 'Kwa Heri'. Katika mashairi haya diolojia imejitokeza upande mmoja, hakuna majibu ya wale ambao mwandishi anazungumza nao. Diolojia hii imekaa katika muundo wa monolojia ya kimaigizo kama anavyoeleza Hurley na O'Neill (2012), kwamba, monolojia ya kimaigizo ni pale mtu mmoja anazungumza akiielekeza hiyo hotuba kwa mtu mwingine au kama anazungumza na nafsi yake mwenyewe. Matokeo ya data katika diwani imebaini mashairi yakitumia muundo wadiolojia ulio katika umbo la monolojia. Katika uundaji wa beti za shairi hili, zinadhihirisha uwepo wa diolojia ambayo inaunda motifu ya msako na motifu ya safari. Mwandishi katika msako wake wa kweli, pia anasaka utulivu na amani ya rafiki yake, ingawa haifahamiki kama rafiki yupo tayari kushirikiana na mwandishi katika msako huo, kwani mwandishi anaeleza kwamba rafiki yake hasikilizi ushauri wa mtu. Diolojia hii katika shairi hili, imeunda motifu ya safari kuu ya mwandishi ya kusaka kweli huku

akitaka wengine nao wafanye hivyo hivyo. Pia mwandishi anamuonya rafiki yake huku akitumia uzoefu aliopata yeye katika safari yake, kwani hakusikiliza ushauri wa ndugu yake hatimaye aliishia kwenye matatizo. Mwandishi anasema:

Nakwambiya hichi change, utakuja nikumbuka
Wambe nali na wenzangu, kitako aloniweka
Akanamba mwendo wangu, niubadili haraka
Lakini sikuyashika, wajipalia makaa (ub. 13)

Kanama yali ni kweli, ni kheri ‘ngemsikiza
Lakini siakuyajali, alo inieleza
Nali fahali fidhuli, kila uchao hifuza
Leo ndiyo naliwaza, wajipalia makaa. (ub. 15)

Katika dondoo hili diolojia inajitokeza pale mwandishi anatumia uzoefu alioupata katika safari yake kama mfano na kiongozi wa maamuzi atakayoyafanya rafiki yake anayetaka kuianza safari. Haijulikani kama safari ya rafiki kama iko sawa na ile aliyoipitia mwandishi, bali inaonekana kwamba mwandishi asingependa rafiki yake aisafiri.

Mwandishi aliendelea kuunda motifu za safari na msako kwa kutumia mbinu ya diolojia katika shairi la ‘Usiniuwe’. Katika shairi hili, mtoto aliyeko tumboni anaongea na mama yake akimsihi asimuue. Aina hii ya diolojia ni diolojia ya ndani kama anavyoeleza Deshpande (2025) kwamba, diolojia ya ndani ni monolojia ya ndani ya wahusika: Mawazo yao, tafakari zao na mjadala wa nafsi; unaonesha kiwango cha hisia na kubainisha kile mhusika anafanya na sababu za kufanya hivyo. Pia, mjadala wa ndani unaonesha hisia zisizoweza kuelezwa kama mashaka, matamanio au hofu. Katika diolojia hii mambo ya ndani yasiyoweza kuelezwa, hufanyika katika kichwa cha mhusika na humsaidia msomaji kumuelewa vizuri mhusika. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha mchomozo wa kimwingilianomatini, ambapo mjadala wa nafsi haufanyiki kichwani kwa mhusika bali tumboni. Tunamwona mtoto anamweleza mama yake kuwa ana haki ya kuishi hata kama hajakamilika kuumbwa. Anaeleza hatua mbalimbali za safari yake ya kuumbwa mpaka anapokamilika akiwa tumboni. Sauti yake imejaa uchungu lakini haijakata tamaa. Kwa mfano, katika ubeti wa 15 na 16 mwandishi anasema:

Ngoja! Usinisongowe, niweke mama niweke
Niweke hadi nikuwe, halafu ndipo ‘tatoka
Kama hunitaki wewe, ulimwengu wanitaka
Mwanayo usiniuwe, mamangu nihurumiya( ub. 15)

Kama hunitaki mama, piya waniuliyani?
Nakuomba nikisema: usiniuwe tumboni
Mama nizaa salama, kisha nitupe ndiyani
Mja alo na huruma, ana’okote kunileya. (ub. 16)

Diolojia katika shairi hili imeunda motifu ya safari na motifu ya msako, kwani kuna safari na msako wa kweli na mapenzi. Safari hii inaanzia mahusiano ya baba na mama, jinsi mimba ilivyotungwa na ukuaji wa mtoto tumboni. Mtoto anamuomba mama yake amuache akamilike kuumbika tumboni kisha azaliwe. Akielezea kuhusu suala la malezi mtoto anasema, sio lazima alelewe na mama yake. Mwandishi ameonesha motifu ya msako iliyoambatana na safari hii, ambapo mtoto aliye tumboni anasaka haki ya kuishi na kutunzwa.

Mwandishi aliandika mashairi mengine yenye msemezano wa nafsi. Katika mashairi hayo, mwandishi alikuwa na diolojia yake binafsi ndani ya shairi yaani monolojia. Mashairi yote yako katika mfumo wa mjadala wa nafsi ingawa yapo yale yaliyoonesha mjadala wa nafsi ulio wazi. Deshpande (2025) anaeleza kwamba monolojia ni hotuba ya mhusika iliyo ndefu na isiyokatishwa. Mara nyingi monolojia hufichua Mawazo binafsi, Imani au hisia. Anaendelea kufafanua kwamba, monolojia inafanikiwa zaidi ikitungwa mhusika anapofanya tafakari ya jambo, akizongwa na hisia mahsusi kama huzuni, hofu, au hasira. Mawazo ya Deshpande yanaendana na matokeo ya utafiti yaliyopatikana katika diwani hii. Mwandishi aliandika diwani hii akijaribu kulinda afya yake ya akili. Mwandishi aliogopa kuchanganyikiwa kwa upweke na maumivu ya moyo. Anazungumza na nafsi yake huku anamwaminisha msomaji kuwa anaongea na mtu aliyeko mbele yake. Kwa mfano, katika shairi la ‘Wasiwasi Enda Zako’ mwandishi anaonesha mapambano ndani ya nafsi yake. Anasumbuliwa na wasiwasi na anapambana kuondokana nao. Mwandishi ana wasiwasi juu ya mambo mbalimbali lakini anataka kukabiliana na hiyo wasiwasi ili aweze kuinua imani yake. Katika ubeti wa nne na nane mwandishi anasema:

Tukaapo wanambiaya, hayawi niyatakayo
Kwamba tamaa ngatiya, nasumbuwa wangu moyo
Kwamba hata hingojeya, hayo niyangojeyayo
Ng’o! siyapati hayo, ni bure najisumbuwa (ub. 4)

Huo urafiki wako, wa kuja niungulisha
Kunipa masikitiko, na mateso yasokwisha
Kutoka leo ni mwiko, sitautaka maisha
Kamwe hutanikondesha, tokomeya mwana kwenda. (ub. 8)

Dondoo hili linamwonesha mwandishi akiongea na nafsi yake ambayo ina wasiwasi, na yeye anataka kukabiliana na wasiwasi huo. Mwandishi anaongea na hisia zake kama vile anafanya mjadala na binadamu mwingine. Anataka kuwa jasiri na kuwa na imani na mawazo yake na mipango yake kwamba itafanikiwa. Lakini wasiwasi unamsumbua, ana hofu ya kutofanikiwa. Mjadala huu wa nafsi ni mbinu mojawapo aliyoitumia mwandishi kuunda motifu za safari na msako wa maisha ya mwandishi kifungoni na motifu za safari na msako wa kusaka kweli. Katika safari na misako hii mwandishi ana hofu ya kufanikisha malengo yake.

Hivyo basi, ingawa mashairi yaliyotumika katika utafiti huu ni yale ya kimaelezo aliyoyaandikwa katika diwani yake ya *Sauti ya Dhiki* (1973) na mwandishi Abdilatif Abdalla, lakini diolojia ya

kimwingiliano matini imejidhihirisha wazi katika mashairi yake na imekuwa ni mbinu mojawapo aliyoitumia kuunda motifu za safari na msako. Mwandishi amekuwa na diolojia ya nafsi na diolojia ya shairi na shairi kati yake na ndugu zake. Pia, amekuwa na mashairi yenye muundo wa barua, ambapo mwandishi anaandika shairi kwa ajili ya kufikisha ujumbe kwa mtu mahususi au kundi la watu mahususi na mwisho mashairi yenye ujumbe kwa jamii. Upande wa pili wa diolojia hii umekuwa ama kujibu kwa shairi ama mwitiko wa mabadiliko kutokana na hali za mambo ambazo mtu mwandishi anapitia au jamii yake. Hivyo basi, diolojia ya matini mbalimbali ndani ya diwani imetumika kama mbinu ya kuunda motifu za safari na msako na kusaidia katika kutimiza lengo la pili la utafiti huu.

**4.3 Mbinu ya Shajara**

Mbinu nyingine iliyotumika kuunda motifu za safari na msako katika mashairi ya kimaelezo katika diwani teule ni mbinu ya shajara. Mbinu hii imeshadadiwa na uwepo wa data zinazoithibitisha kutoka katika diwani teule. Kwa mujibu wa Mulokozi (2017), shajara ni moja ya sanaa ya kale ambayo ni kitabu cha kumbukumbu za matukio ya kila siku. Pia, anaeleza kwamba uandishi wa shajara uliota mizizi karne nyingi sana kabla ya ugunduzi wa riwaya. Anaendelea kufafanua kwamba, shajara ni moja ya sanaa ambayo iliathiri utunzi wa riwaya za kisira. Mulokozi anathibitisha maelezo yake kwa kuwarejelea Wellek na Warren (1949) ambao wanasema: "Kabla ya kufikia ukomavu katika hadithi za Pamela, Tom Jones na Tristram Shandy, riwaya ilitanguliwa na fani sahili kama barua, shajara, masimulizi ya wasafiri, kumbukumbu". Mtafiti Ash (2023) anaendelea kufafanua shajara kuwa ni rekodi ambayo kiasilia iliandikwa kwa mkono ikihusu mambo muhimu yanayoelezea maisha binafsi ya mtu ya kila siku au kwa kipindi cha muda fulani. Anaendelea kueleza kuwa, ni mahali ambapo unaweza kuwa mkweli kwako mwenyewe na kuandika mawazo yako na tafakari zako juu ya mambo yaliyotokea karibu na wewe, ukiachana na vikwazo vyovyote toka nje.

Matokeo ya utafiti huu yamebaini kuwa, matumizi ya shajara si mbinu iliyoathiri uandishi na utunzi wa riwaya tu kama Mulokozi (2017) na wataalamu wengine walivyoeleza, bali ni mbinu ambayo mwandishi Abdilatif Abdalla ameitumia pia katika utunzi na uandishi wa diwani yake ya *Sauti ya Dhiki* (1973). Mbinu hii ni ya kimwingiliano matini, kama Zengin (2016) anavyoeleza kwamba matini zote zinaingiliana kwa sababu zinarejelea, zinanukuu na kuiga kutoka katika matini zilizotangulia. Mwandishi anapoandika kazi yake mwingilianomatini unaweza ukajitokeza kwa bahati mbaya ndani ya matini yake, kwa uchaguzi au kwa kulazimika. Katika utafiti huu, imebainika kuwa mwandishi ametumia njia ya mwigo wa kimwingiliano wa matini wa mbinu za uandishi wa matini ulioanza tangu zamani. Mwandishi ametumia mbinu hii kwa kuandika tarehe, mwezi na mwaka au mwezi na mwaka aliotunga katika kila shairi. Mashairi haya yamepangwa kwa muundo huo, yakianza yale aliyoandika mwanzoni mwa uandishi wake akiwa kifungoni, mpaka lile aliloandika baada ya kutoka kifungoni. Mwandishi alipangilia mashairi yake ya kimaelezo kwa kuanza na shairi la 'N'shishiyelo ni Lilo' aliloliandika Septemba 1969. Shairi la pili la kimaelezo aliloliandika mwandishi ni shairi la 'Kamliwaze' aliloliandika Oktoba 1969. Shairi la tatu ni shairi la 'Tuza Moyo' aliloliandika Novemba 1969 na shairi la nne ni shairi la 'Jipu' aliloliandika Januari 1970. Mwandishi hajaandika ni tarehe ngapi aliandika mashairi haya. Katika miezi hii mitano, kutoka Septemba 1969 mpaka Januari 1970, mwandishi aliandika mashairi manne tu.

Mashairi mengine ya kimaelezo aliyoyaandika mwandishi ni kama yafuatayo: shairi la kumi na moja la kimaelezo lililoitwa 'Telezi' liliandikwa tarehe 3 Agosti 1970. Shairi lingine la kumi na mbili la kimaelezo ni shairi la 'Semeni Wenye Kusema' lililoandikwa tarehe 19 Oktoba 1970. Mwezi huo huo wa Oktoba mwandishi aliandika shairi lingine la kumi na tatu la 'Muwerevu Hajinyowi' tarehe 27 Oktoba 1970. Mwezi Novemba mwandishi aliandika mashairi matatu ya kimaelezo ambayo ni: shairi la kumi na nne linaloitwa 'Yatakoma' lililoandikwa tarehe 3 Novemba 1970, shairi la kumi na tano la 'Ah! Mwenzangu' lililoandikwa tarehe 17 Novemba 1970. Shairi lingine la kimaelezo lililoandikwa Novemba ni shairi la kumi na sita linaloitwa 'Wasiwasi Enda Zako' lililoandikwa tarehe 23 Novemba 1970.

Mwezi Januari mwaka 1971 mwandishi alitunga mashairi matatu ya kimaelezo; mashairi hayo ni shairi la kumi na saba 'Mja si Mwema' lililoandikwa tarehe 10 Januari 1971. Shairi lingine la kumi na nane ni 'Lipi Litakalokuwa' lililoandikwa tarehe 14 Januari 1971 na la mwisho ni shairi la kumi na tisa linaloitwa 'Mamaetu Afrika' lililoandikwa tarehe 29 Januari 1971. Mwezi Februari alitunga shairi moja tu la kimaelezo, ambalo ni la ishirini linaloitwa 'Jana na Leo na Kesho', aliliandika tarehe 12 Februari 1971.

Mwezi Machi mwandishi alitunga mashairi mawili tu ya kimaelezo, ambapo alitunga shairi la ishirini na moja linaloitwa 'Chema Hakidumu' tarehe 15 Machi 1971 na alitunga shairi la ishirini na mbili linaloitwa 'Moyo Iwa na Subira' alilolitunga tarehe 20 Machi 1971. Mwezi Aprili alitunga shairi moja tu la ishirini na tatu linaloitwa 'Usiniuwe!' Alilolitunga tarehe18 Aprili 1971. Katika mwezi Mei mwandishi alitunga shairi moja tu la kimaelezo ambalo ni la ishirini na nne linaloitwa 'Mambo Yana Mambo Yake', alilitunga tarehe 9 Mei 1971. Mwezi juni mwandishi alitunga mashairi matatu ya kimaelezo ambayo ni, shairi la ishirini na tano linaloitwa 'Watiliye Pamba' lililotungwa tarehe 1 Juni 1971. Shairi lingine ni shairi la ishirini na sita linaloitwa 'Tendekezo' alilotunga tarehe 28 Juni 1971 na shairi la ishirini na saba linaloitwa 'Leo N'singekuwako' alilotunga tarehe 14 Juni 1971. Shairi la ishirini na sita pamoja na lile la ishirini na saba yana mpangilio tofauti na mashairi mengine yaliyoandikwa zaidi ya moja ndani

ya mwezi mmoja, kwani mashairi yote yamekaa kwenye fomula moja, yanaanza yale ya tarehe za mwanzo wa mwezi na kuendelea tarehe zinazofuata katika mwezi husika. Lakini mashairi haya mawili hayajafuata mpangilio husika, hivyo yanaleta picha ya kukosewa kupangiliwa au mwandishi; alikosea kuandika tarehe kwenye shairi la ishirini na sita.

Mwandishi alitunga shairi moja tu la kimaelezo katika mwezi Julai ambalo ni shairi la ishirini na nane linaloitwa ‘Kokoiko’, lilitungwa tarehe 3 Julai 1971. Mwezi Septemba mwandishi alitunga mashairi ya kimaelezo matatu ambayo ni shairi la ishirini na tisa linaloitwa ‘Sikakawane na Kimya’ alilolitunga tarehe 5 Septemba 1971. Shairi lingine ni la thelathini linaloitwa ‘Wasafiri Tuamkeni’, alilolitunga tarehe 4 Septemba 1971 na la mwisho ni shairi la thelathini na moja linaloitwa ‘Zindukani’ alilolitunga tarehe 22 Septemba 1971. Katika mashairi yaliyotungwa mwezi huo, unaonekana tena makosa ya mpangilio wa tarehe kati ya shairi la thelathini na lile la thelathini na moja. Mwezi Oktoba, mwandishi alitunga shairi moja tu la kimaelezo. Shairi hili la thelathini na mbili linaitwa ‘Kwa Heri’ lilitungwa tarehe 9 Oktoba 1971.

Katika mwezi Novemba mwandishi alitunga mashairi mawili ya kimaelezo. Alitunga shairi la thelathini na tatu lenye jina ‘La Mjini na La Shamba’. Shairi hili lilitungwa tarehe 2 Novemba 1971. Shairi lingine ambalo ni la thelathini na nne ni shairi la ‘Muosheni’ ambalo alilitunga tarehe 19 Novemba 1971. Katika mwezi Disemba mwandishi alitunga shairi moja la kimaelezo ambalo ni shairi la thelathini na tano, shairi hilo linaitwa ‘Naja’, liliandikwa tarehe 19 Disemba 1971. Mwisho, mwandishi aliandika shairi la thelathini na sita la kimaelezo akiwa bado kifungoni lenye jina la ’Ndiya Panda’, aliliandika tarehe 23 Januari 1972.

Mbinu hii imeunda motifu za safari na msako wa maisha ya mwandishi kifungoni, imani yake katika kweli na kukua kwake kififikra na kimtazamo. Pia, imetoa picha ya ubinadamu wa mwandishi, akionesha hisia za kujiamini, kukata tamaa, kujilaumu, kuhisi kusalitiwa, kupenda na kadharika. Kama ilivyoainishwa katika lengo la kwanza, imebainika picha ya hali ya mwandishi akiwa kifungoni siku baada ya siku au mwezi baada ya mwezi au mwaka baada ya mwaka. Katika diwani, imeonekana safari yake ya mabadiliko kisaikolojia au kifikra na kimtazamo. Hivyo kwa kupitia mbinu hii motifu zote za safari na msako zilizobainishwa katika lengo la nne zimeundwa.

**4.4 Mbinu ya Kisitiari**

Sitiari ni mfumo wa akili ambao unaturuhusu kutumia kile tunachokifahamu, na kutumia uzoefu wetu kuhusu mazingira na jamii kwa ajili ya kuelewa dhana zingine mbalimbali (Lakoff, 1980). Anaendelea kueleza kwamba, kwa sababu sitiari hizo zinaunda msingi wa uelewa na uzoefu, hivyo basi, hizo ni sitiari tunazoishi nazo, sitiari ambazo zinaunda mitazamo na matendo yetu bila ya sisi kuzitambua. Utafiti huu unatofautiana na mawazo ya Lakoff hasa anapoeleza kwamba sitiari ni mfumo wa akili, kwani utafiti huu umezitazama sitiari kama mbinu ya lugha. Kahigi (2020) anaendelea mbele na kusema, sitiari ni kipengele cha kisemantiki ambacho kwa kawaida hujumuishwa katika taswira au tamathali. Taswira ni kipengele chochote cha lugha kinachoibua maono mahususi (au picha) akilini mwa mpokeaji yeyote wa fasihi kupitia kwenye milango yake ya fahamu hadi mtu huhisi kuwa anaona, anagusa, anaonja, anasikia au ananusa kitu kilichosawiriwa. Maono au picha hiyo huweza kuibushwa na neno, fungu la maneno, matini ndogo katika matini kubwa (kama vile shairi zima au hadithi au matini yoyote ndefu ya kifasihi au ya aina nyingine. Pia, anasema, sitiari ni kipengele kinachohamisha maana kutoka kikoa kimoja kwenda kingine. Kahigi anaeleza kwamba sitiari inaundwa na vipengele vitatu ambavyo ni kitajwa, kifananisho na kiungo (sifa au tabia zinazounganisha kitajwa na kifananisho). Mbinu ya kisitiari ni mbinu mojawapo aliyoitumia mwandishi kuunda motifu za safari na msako katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* (1973) ya Abdilatif Abdalla. Motifu za safari na msako zimeundwa na mwandishi kwa kutumia mbinu hii ya sitiari katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* (1973), kwa kupitia mashairi mbalimbali kama yafuatayo: shairi la ‘Jipu’, ‘Mamba’, ‘Wasafiri Tuamkeni’, na ‘Telezi’ tukiyataja kwa uchache.

Katika shairi la ‘Jipu’ mwandishi anatumia taswira ya jipu kuelezea yanayomsibu. Mwandishi anaeleza uchungu na maumivu makali anayoyapata kutokana na jipu lililomuota makalioni. Mwandishi anaeleza kuwa ingawa ana maumivu makali sana na uchungu lakini anasubiri siku ifike ambayo ataweza kulikamua litoe usaha na damu yote kisha auguze jeraha kwa dawa na mwisho apone. Mwandishi anasema:

Siku ya kuiva kwake, hiyo ndiyo siku kweli
Huo ndiwo mwisho wake, na mwisho wa idhilali
Idhilali in’ondoke, mimi nayo tuwe mbali
Siku hiyo ni mawili, kuteka au kuliya (ub.8)

Baada ya yote haya, jaraha niliuguze
Kwa madawa kulitiya, ili kwamba yalipoze
Irudi yangu afiya, na zaidi niongeze
Nirukeruke niteze, kwa furaha kuningiya. (ub.11)

Katika dondoo hili tunamwona mwandishi aliyetumia taswira ya jipu kuonesha jinsi anavyoisubiri siku ya kumaliza kifungo na mabadiliko ya jamii katika imani juu ya kweli kwa furaha. Katika safari ya mwandishi ya kifungo, amekutana na madhira mengi na anasubiri siku ya kifungo chake kuisha. Katika dondoo mwandishi anaingoja siku ya jipu kuiva na anasema kuna mawili anayoyatarajia siku hiyo kucheka au kulia. Atalia kwa ajili ya maumivu ya kukamua jipu lakini pia atacheka kuondokana na jipu hilo. Anaamini kuwa msako wake utafanikiwa mwishoni, katika mistari hii mwandishi anajua kuwa kuna siku maumivu ya kifungo yataisha na kile anachokisaka atakipata. Hivyo basi,

katika safari ya kifungo cha mwandishi inaonekana kwamba mwandishi anaamini katika kusaka kweli. Pia, mwandishi anaamini kuwa, yoyote yule aliye kinyume naye kuna siku mwisho wake utafika.

Mwandishi aliandika shairi lingine lililotumia mbinu ya sitiari kuunda motifu za safari na msako katika diwani hii. Shairi hilo aliliita 'Wasafiri Tuamkeni'. Katika shairi hili mwandishi ametumia taswira ya safari ya kawaida kuelezea safari ya mapinduzi katika jamii yake. Katika mshororo wa mwisho wa kila ubeti mwandishi anasema: 'Huu ndiwo mwanzo wake, siwo mwisho wa safari'. Mambo aliyokumbana nayo yeye, sababu ya kuianza hiyo safari mpaka kuishia kifungoni, ni mambo ambayo kiuhalisia ni rahisi kuwakatisha tamaa wale waliokuwa na imani na msimamo kama wa mwandishi. Lakini, yeye bila kutaja ni nini, anasema huo ni mwanzo na si mwisho. Mawazo haya yamedhihirika katika ubeti wa mwisho, anaongea na kiongozi wa safari hiyo ya mapinduzi, anasema:

Na mshika bendera, kwa vizuri naishike
Daima nawe imara, wala asilainike
Ay'ongoze barabara, huko twendako tufike
Huu ndiwo mwanzo wake, siwo mwisho wa safari. (ub. 13)

Sitiari ya mshika bendera aliyoitumia mwandishi inatoa taswira ya kiongozi wa msafara katika safari hii ya kimapinduzi. Shairi hili linaunda motifu ya safari na msako kwa kuendelea kuonesha safari ya mwandishi ya kusaka kweli pamoja na safari ya wasafiri wenzake wanaopigania kweli kama yeye.

Mwandishi alitumia pia mbinu ya sitiari katika kuandika shairi la 'Telezi'. Mwandishi ametumia taswira ya mvua kubwa iliyonyesha na ikaacha maji na matope mengi barabarani. Mwandishi ametumia sitiari ndani ya shairi hili, na kuunda motifu za safari na msako wa maisha ya wandishi kifungoni, safari na msako wa wakulima na safari na msako wa kusaka kweli.TheProsePath (2025) wanaeleza kwamba, sitiari ya mafuriko katika fasihi inamaanisha mabadiliko, ghasia na kuzaliwa upya. Wanaendelea kueleza kuwa taswira ya mafuriko inafafanua jinsi nguvu zinazotumika kubadilisha wahusika na dunia yao, pia inamaanisha uharibifu na uwezekano wa kuwepo kwa mwanzo mpya. Maana hii inapishana kwa kiasi kikubwa na yale yaliyoelezwa na mwandishi katika shairi hili, tunaona mvua ambayo iliwatisha watu wengi, ikasababisha wengine kukimbilia upenuni na wengine kukimbilia majumbani na kujifungia. Mvua hiyo iliwaletea hasara wakulima lakini pia baada ya kuisha inaacha matope mengi barabarani yanayosababisha watu kuanguka. Mwandishi anasema:

Mimea waloipanda, ilitekukatekuka
Kazi ngumu walotenda, yote ikaharibika
Hawakuvuna matunda, waliyo wakiyataka
Waliyo wakiyataka, yakawa ya mbali nao. (ub.2)

Katika dondoo hili mwandishi ametumia taswira ya mvua kubwa kama uongozi wa kimabavu uliokuwa katika jamii yake, wakulima kama wananchi ambao walikuwa na matumaini mengi na matokeo ya uhuru waliishia kuvunjika mioyo na kupata hasara. Mvua iliyonyesha ikiwa kama uongozi mpya ilikuwa mbaya, kwani mvua kwa mkulima inatakiwa kuwa baraka na msaada kukuza mazao, bali mvua hii iliyaharibu mazao yote shambani. Mwandishi anaeleza jinsi alivyojaribu kutembea kwenye njia iliyojaa matope baada ya mvua kuisha, akaishia kwenye utelezi. Kama anavyoeleza katika ubeti wa 6 na 7, mwandishi anasema:

Japo hivyo zilikuwa, ndiya hazipitiki
Bali mimi haamuwa, kwenenda japo kwa dhiki
Kumbe vile nitakuwa, ni mfano wa samaki
Ni mfano wa samaki, kuiendeya ndowana (ub.6)

Zikanibwaga telezi, sikujuwa kuzendeya
Ningekwenda kwa henezi, yasingenifika haya
Lakini tena siwezi, mwendo huo kutumiya
Sitawata kutembeya, ila tabadili mwendo. (ub. 7)

Katika dondoo hili mwandishi anaonesha shida aliyoipata baada ya kutembea njiani baada ya mvua kukoma. Ingawa mwandishi alionesha jinsi watu katika jamii yake walivyokuwa waoga, wakikimbia na kujificha upenuni au kujifungia ndani, wakiogopa mvua, anaeleza jinsi yeye alivyokuwa na ujasiri wa kuingia barabarani kuanza safari na kukabiliana na matope na utelezi. Mwandishi anagundua njia aliyoitumia haikuwa sahihi ndio maana akaishia kuteleza. Ingawa aliteleza katika njia ya kwanza hajakata tamaa, yupo tayari kuendelea kutembea lakini anataka kubadili mwendo. Hii ni taswira ya kile kilichompata mwandishi katika harakati zake za kupambana na uongozi mbaya unaonesha anaishia kifungoni, sawa na alivyoteleza kwenye utelezi baada ya kutoka kukabiliana na njia iliyojaa tope.

Shairi hili linaendeleza muundo wa safari na msako wa kweli alioundea mwandishi mpaka ukamsababisha akaishia kifungoni. Lakini katika safari hii, mwandishi hajakata tamaa, yupo tayari kuendelea na mapambano hata baaada ya kufungwa, lakini kama alivyoeleza katika ubeti wa saba anasema ataendelea na mapambano lakini atabadili mwendo ili asije akaishia kwenye utelezi kama ilivyokuwa katika safari ya mwanzo. Mwandishi ametumia mbinu hii ya kisitiari katika kuunda motifu hizi za safari na msako. Mbinu hii imedhihirisha uwezekano wa uwepo wa motifu za safari na msako katika mashairi ambayo ni ya kimaelezo tofauti na ilivyokuwa ikizoeleka hapo awali kuwa zinapatikana katika mashairi ya kimasimulizi na drama.

### 4.5 Mbinu ya Sauti ya Usimulizi

Hii ni mbinu nyingine anayoitumia mwandishi kujenga motifu za safari na msako katika diwani ya *Sauti ya Dhiki*. Sauti ya usimulizi inaelezwa kama nafsi inayotumika kusimulia matukio ndani ya kazi ya fasihi (Mahenge, 2018). Mbinu hii husaidia kujua mtazamo wa mwandishi juu ya masimulizi na nia ya kusimulia. Mahenge anaendelea kueleza kuwa ni muhimu kufahamu nani anayesimulia katika hadithi kwani kupitia

hilo tutajua mtazamo wake. Anaeleza kuwa msimulizi anaweza kuwa ni msimulizi mhusika, msimulizi aliye nje ya usimulizi, au wakala anayeachwa na msimulizi ili asimulie badala yake.

Kwa mujibu wa Genette (1980), Bordwell (1985) na Bal, (1997) wataalamu ambao walieleza misingi mitatu ya Nadharia ya Naratorojia, moja ya misingi yao waliyoibanisha ni usimulizi, hadithi, na ploti. Wanasema, katika msingi wa usimulizi, tunajiuliza "ni kwa vipi" hadithi inasimuliwa, yaani, kwa mtazamo wa nani hadithi inasimuliwa. Hapa ina maana ya "sauti" za usimulizi zinazotumika katika kusimulia jambo, kama ni kwa nafsi ya kwanza, pili au tatu. Katika msingi huu wa usimulizi, kila nafsi inayotumika kusimulia ina maana yake. Kwa kutumia nafsi ya kwanza, ina maana kuwa msimulizi yuko karibu na simulizi na pia yuko hai zaidi. Kwa kutumia nafsi ya pili, ina maana kuwa msimulizi yuko hai na yuko karibu na simulizi lakini anamshirikisha msomaji ili naye abebe majukumu fulani katika hadithi. Nafsi ya kwanza na nafsi ya pili ziko katika darajia la kwanza ambalo linafungamana na nafsi ya mwandishi.

Kwa kiasi kikubwa katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* uandishi wa mashairi, hasa yale ya kimaelezo, mwandishi anatumia nafsi ya kwanza umoja kueleza hali yake aliyokuwa anakabiliana nayo akiwa kifungoni. Kwa sababu ya matumizi ya nafsi hii, inajulikana kwamba tungo zilizopo ndani ya mashairi hayo zinamhusu mwandishi moja kwa moja. Kwa mfano katika shairi la kwanza la 'N'shishiyelo ni Lilo' mwandishi anaanza ubeti wa kwanza na wa nne kwa kusema:

Nipulikiza ndu yangu, ninenayo usikiye
Yaliyo moyoni mwangu, ningependa nikwambiye
Ujuwe Imani yangu, ambayo niishishiye
Siiwati ingawaye, n'shishiyelo ni lilo (ub. 1)

Kweli imenitongeya, kwa kuinena mwendani
Wale nalowaambiya, wamenitiya dhikini
Wameniona mbaya, kumshinda Firauni
Kweli, sasa naamini, si wangi waipendao. (ub. 4)

Katika beti hizo mwandishi anaanza kwa kumuandaa ndugu yake atulie kumsikiliza kisha anamwambia sababu ya masimulizi anayotaka kuyatoa. Masimulizi anayoyatoa yanahusu imani yake katika kweli ambayo ameishikilia na hayuko tayari kuiacha. Kutokana na masimulizi haya, inajengeka safari ya mwandishi ya kifungo pamoja na safari ya mwandishi ya kupigania kweli. Safari hizi zimeendelea kujengwa na mwandishi kupitia mashairi yake mbalimbali ndani ya diwani. Mashairi hayo ni kama yafuatayo: 'Kamliwaze', ambalo mwandishi ametumia nafsi ya kwanza umoja na wingi anapozungumza juu yake na ndugu yake; pia, ametumia nafsi ya pili umoja anapozungumza na mtumishi wake. Shairi lingine ni shairi la 'Tuza Moyo' ambalo mwandishi ametumia nafsi ya kwanza umoja na nafsi ya pili umoja akizungumza na kaka yake. Shairi lingine la kimaelezo ni 'Jipu'. Katika shairi hili mwandishi ametumia nafsi ya kwanza umoja akieleza shida anazopambana nazo kwa sababu ya jipu. Mwandishi anasema:

Nna jipu lintunza, linipalo tabu mno
Tangu liliponianza, kamwe sipati usono
Kwamba ni mara ya kwanza, kuuguwa ndwezi hino
Latoma kama sindano, utunguwe nakwambiya (ub. 3)

Mashairi mengine ya kimaelezo yanayotumia nafsi ya kwanza ni shairi la 'Siwati', 'Mamba', 'Nakukumbuka', 'Ukamilifu wa Mja', 'Lililokuudhi ni Lipi?', 'Kuno Kunena', 'Telezi', 'Yatakoma', 'Ah! Mwenzangu', 'Wasiwasi Enda Zako', 'Mja si Mwema', 'Lipi Litakalokuwa', 'Mamaetu Afrika', 'Chema Hakidumu', 'Moyo Iwe na Subira', 'Usiniuwe', 'Watiliye Pamba', 'Leo N'singekuwako', 'Sikakawe na Kimya', 'Wasafiri Tuamkeni', 'Zindukani', 'Kwa Heri', 'Naja, na' 'Ndiya Panda'. Katika mashairi haya ambayo mwandishi ametumia nafsi ya kwanza, mengi yupo katika diolojia na nafsi yake mwenyewe, ndugu zake, rafiki zake na jamii yake kwa ujumla. Hivyo, mashairi mengi yametumia nafsi ya kwanza umoja na wingi na mengine yametumia nafsi ya kwanza na nafsi ya pili. Muundo wa sauti ya usimulizi katika mashairi haya yamesaidia kuundwa kwa safari na motifu mbalimbali katika diwani hii kama zilivyoainishwa katika sura ya kwanza nne na tano ya utafiti huu.

**4.6 Hitimisho**

Makala hii imebaini mbinu mbalimbali ambazo ni za kimwingilianomatini zilizotumiwa na mwandishi kuunda motifu za safari na msako katika diwani hii. Mbinu hizi ni tofauti na mbinu zilizojikita na aina za tamathali za semi ambazo zimekuwa zikichambuliwa na tafiti zilizotangulia (Mligo, Mutembei, Kadallah 2024; Odhiambo, wa Mutiso na Wamitila, 2024). Mbinu zilizobainishwa katika Makala hii ni kama zifuatavyo: kwanza mwandishi ametumia mbinu ya ruwaza. Katika mbinu hii amepangilia mashairi katika ruwaza kama ilivyo katika Nadharia ya Ruwaza ya Shujaa. Pili, mbinu nyingine iliyoainishwa ni mbinu ya udiolojia. Katika mbinu hii mwandishi ameandika mashairi ambayo yanajibizana na mashairi mengine ambayo alikuwa anayapata kutoka kwa ndugu zake. Mbinu ya tatu ni shajara. Katika mbinu hii mwandishi ameyapangilia mashairi yake kama shajara, ambapo msomaji anakuwa anajua mambo yaliyokuwa yanaendelea katika vipindi fulani vya maisha yake. Mashairi yameandikwa kwa mpangilio wa tarehe, mwezi na mwaka au mwezi na mwaka. Mbinu nyingine iliyotumika ni mbinu ya sitiari. Mashairi mengi aliyoandika mwandishi yametumia sitiari kufikisha ujumbe wake. Mwisho, ni mbinu ya sauti ya usimulizi. Katika mbinu hii sauti ya mwandishi ndiyo iliyotawala kwani katika mashairi mengi aliyoyaandika ametumia nafsi ya kwanza umoja na uwingi pamoja na nafsi ya pili umoja na uwingi. Yakiwa ni mashairi ambayo anaelezea uzoefu wa maisha yake kifungoni au akizungumza na ndugu, rafiki na wanajamii yake walioko nje ya gereza. Ingawa mwandishi hakuweka

bayana kama ni mbinu alizozitumia kwa kudhamiria au kutokudhamiria kama anavyoeleza Kristeva (1980), lakini mwandishi ametumia mbinu za kimwingiliano matini katika utunzi na uandishi wa kazi yake. Mbinu hizi zilimsaidia kuipa upekee diwani yake na kuweza kufikisha ujumbe kwa walengwa pasi na kuleta shida. Mathalani, alitumia mbinu ya dialojia kuwaandikia ndugu na marafiki zake kama barua pasi na kutambulika. Kama alivyoeleza aliandika mashairi haya kwa njia ya misimbo ambayo haikueleweka na kila mtu.

## MAREJELEO


- Abdalla, A. (1973) *Sauti ya Dhiki*. Nairobi: Oxford University Press.
- Ash, J. (2023) Diary: Definition, Examples and Meaning, Inapatikana katika https://www.englishliterature.info/2023/08/diary-definition-examples-meaning.html. Ilisomwa tarehe 6/02/ 2023.
- Bal, M. (1997). *Narratology Introduction to the Theory of Narrative*. 2nd edn. Toronto: University of Toronto Press.
- BBC (2025) 'Pattern- AQA' Inapatikana katika https://www.bbc.co.uk/bitesize/guides/z3c4jty/revision/1 Ilisomwa tarehe 11/02/2025
- Bordwell, D. (1985). *Narration in the Fiction Film*. Madson: University of Wisconscin Press.
- Brewster, S. (2009) *Lyric, New Critical Idiom*, London, Routledge
- Campbell, J. (1973) *The Hero with a Thousand Faces.* Bolingeu*:* Princeton.
- Deshpande, S. (2025) 5 Types of Dialogue and How to Use Them in Fiction, Inapatikana katika https://nownovel.com/types-of-dialogue/ Ilisomwa tarehe 17/10/ 2023
- Fiveable Inc. (2024) Quest Motif: Middle English Literature, Inapatikana katika https://library.fiveable.me/key-terms/middle-english-literature/quest-motif. Ilisomwa tarehe 16 /10/ 2024
- Freedman, W. (1971) The Literary Motif: A Definition and Evaluation, *NOVEL: A Forum on Fiction*, Vol. 4, No. 2 (Winter, 1971), pp. 123-131, Duke University Press.
- Genette ,G. (1980). *Narrative Discourse: An Essay on Method.* Trans. Jane E. Lewin. Ithaca: Cornell University Press.
- Kahigi, K. K. (2020). "Sitiari Katika Kichomi- Uchambuzi wa mojawapo ya Mbinu za Kifasihi ya Euphrase Kezilahabi" *Swahili Forum 27 (2020)* 32-56) https://www.researchgate.net/publication/35675506_SITIARI_KATIKA_KICHOMI_UCHAMBUZI_WA_MOJAWAPO_YA_MBINU_ZA_KIFASIHI_YA_EUPHRASE_KEZILAHABI
- Kristeva, J. (1980). *Desire in Language: A Semiotic Approach to Literature and Art*. (Ed. Leon S. Roudiez, Transl. Thomas Gora, Alice Jardine and Leon S. Roudiez), Columbia University Press, New York
- Kristeva, J. (1990). *Desire in Language. A Semiotic Approach to Literature and the Arts*. Thomas Gora, Alice and Leon (Trans) New York. Columbia University Press.
- Kunene, D. P. (1985) "*Journey as Metaphor in Africa Literature"* Stephen A. Mh. *African Literature Studies:* The Present State/L" et al., Present. Washington: Three Continents Press.
- Lakoff, G, na Johnson, M. (1980) Metaphors We Live By, Chicago: University of Chicago Press
- Mahenge, E. (2018). "Uumbaji wa Ualbino Katika Fasihi ya Kiswahili: Uchambuzi wa Kazi Teule". Tazimili ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).
- Mligo, W. Mutembei, A. na Kadallar, R.T. (2024) Uchunguzi wa Mtagusano baina ya Hisia na Motifu: Mifano kutoka Tamthilia ya *Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe*. *Mulika* No.43(2), 336-350. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mulokozi, M. M. (2017) *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam : KAUTTU.
- Mung'aya, Y. (2018) "Narratological Significance of Journey Motif in Severine Ndunguru's *A Wreath for Fr. Mayer"*. Tazimili ya Umahiri (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Nyongesa, A. W. (2014) "The Journey Motif; A Study of Nadifa Mohamed and Sati Abdi". Tasinifu ya Umahiri (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Odhiambo, A.R, wa Mutiso, K. na Wamitila, K. W. (2014) 'Mtindo wa Usambamba katika Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi' *Kioo cha Lugha, Juz. 22(1), 123-136* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Pfister, M. (1998) "The Philosophical and the Dramatic Dialogue with Illustrations of the Berlin Production of the Symposium Jean-Jacques Lecercle 'speaking is dirty, writing is clean': The Rules of Dialogue" katika Comparative Criticism An Annual Journal Philosophical Dialogue Volume 20, Cambridge University Press, United Kingdom.
- Raglan, L. (1979) *The Hero.* New York: Median.
- Sosoo, K. S. (2018) "Ushujaa Katika Motifu ya Safari Ya Msako: Ulinganishi wa Ngano za Kiewe kutoka Ghana na Riwaya za Shaaban Robert kutoka Tanzania". Tazimili ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.
- TheProsePath (2025) 'What Does a Flood Specifically Symbolize in Literature' The Prose Path, Inapatikana katika https://youtu.be/_SwXVzjJRNg?si=pmqF3-K6HyG7AMLK ilisomwa tarehe 01/10/2025.
- Vendler, H. (2002) *Poems, Poets, Poetry: An Introduction and Anthology*, 2nd edn. Boston:Bedford/St Martin's, P.xlii.

- Wellek, R. na Warren, A. (1949) *Theory of Literature*. United State of America: Harcourt, Brace and Company, INC.
- Wheeler, L. K. (2018) "Literary Terms and Definitions". Inapatikana katika https://web.cn.edu/kwheeler/lit_terms_Q.html, Ilisomwa tarehe 22/07/ 2020.
- Zengin, M. (2016) "An Introduction to Intertextuality as a Literary Theory: Definitions, Axioms and the Originators". pamukkale Universitesi, Sosyal Bilimler Enstitusu-Dergisi, Sayi 25/1, 2016, Sayfa 299-326 Inapatikana katika http://dergipark.gov.tr/download/article-file/411869 Ilisomwa tarehe 20/03/ 2019.


**Cite This Article:** Nkinde Mwangoka, Aldin K. Mutembei, Elizabeth Godwin Mahenge (2025). Mbinu Zinazotumika Kuunda Motifu za Safari na Msako Katika Mashairi ya Kimaelezo: Mifano Kutoka Katika Diwani ya *Sauti ya Dhiki* (1973) ya Abdilatif Abdalla. *East African Scholars J Edu Humanit Lit, 8*(12), 625-638.